**JINA: ……………………………………………. NAMBARI: ………………………………**

**SAHIHI: ………………………………….. TAREHE: ………………………………..**

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**JUNI 2014**
**MUDA: SAA 2 ½**

# COMA JOINT EXAM 2014

**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**MUDA: 2 ½**

## MAAGIZO

1. Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
4. Hakikisha ya kwamba maswali yote yamo.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Watu wengine hawawezi kunywa chai au uji bila kutia sukari. Wanatumia sukari kwa hamu na ghamu bila kutambua kuwa hiyo ni sumu wanayojiongezea mwilini.

Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wa jadi waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko sisi. Hii ni kwa kuwa waliishi katika kipindi ambacho sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. Iwapo ilikuweko, ilikuwa bidhaa ya wateule waungwana kutengenezea vitu kama keki, mahamri, vitumbua na kadhalika na akina yahe hawangeweza kuigharamia.

Watafiti wa masuala ya afya wamegundua kuwa sukari inayotayarishwa viwandani sasa haina virutubishi vyovyote . Halikadhalika, utaratibu wa viwandani wa kutayarisha sukari ili iwe nyeupe na kuichuja huharibu virutubishi vinavyoweza kuwa muhimu mwilini. Umuhimu wa sukari wakausaza kwa kutia ladha tamu tu. Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii. Baada ya kusagika mwilini, sukari hii huacha masalio ya asidi mwilini yenye sumu inayoathiri siha.

Matumizi ya sukari kwa wingi husababisha madhara mbalimbali mwilini. Kwanza, huchangia kuoza na kuharibika kwa meno pamoja na matatizo ya meno kuuma. Pili, sukari nyeupe imehusishwa na ongezeko la maradhi ya kisukari, moyo na hipoglisimia au upungufu wa sukari mwilini. Matumizi holela ya sukari huleta kipandauso au ugonjwa wa gahfla wa kuumwa upande mmoja wa kichwa unaoambatana na kichefuchefu, kutapika na matatizo ya kuona. Pia ,sukari huleta maradhi ya ngozi na figo, pamoja na ongezeko la kemikali iitwayo kolestroli, ambayo ni ufuta unaonata na ambao unatokana na kutoyeyuka kwa mafuta yote mwilini. Kemikali hii ya kolestroli inaporundikana moyoni, hufanya mishipa inayotoa damu moyoni na kuisambaza mwilini kuwa myembamba na sugu. Moyo hulazimika kusukuma damu kwa nguvu na huenda moyo ukachoka na kukoma kufanya kazi.

Madhara haya ya sukari ndiyo yanayowafanya watu wengi kukiri kuwa sukari, ingawa ni tamu, ni sumu mwilini. Wataalamu wa lishe wamependekeza ulaji wa vyakula kama nafaka, matunda, mboga na miwa ambavyo vimejaa sukari asilia.

Fauka ya hayo, sukari inayotoka katika asali ni bora zaidi kwa mwili wa mwanadamu. Asali huwa na sukari asilia,vitamini, madini na amino asidi. Hivi vyote huwa na manufaa mbalimbali mwilini. Mathalani, asali huupa mwili nishati inayohitajika kuendesha shughuli za viungo. Licha ya hayo, asali huuchangamsha mwili. Asali huwa na kemikali ambazo husaida watoto kukua vizuri. Huweza kuzidisha kiwango cha himoglobini, hivyo kupunguza uwezekano wa watoto kuwa na anemia ( upungufu wa damu ) . Halikadhalika, asali husaidia katika usagaji wa chakula iwapo itatumiwa kabla ya mlo. Matumizi ya kijiko kimoja cha asali kila siku husaidia mwili kujikinga dhidi ya magonjwa ya kukohoa. Asali husaidia pia kuondoa harufu mbaya kinywani.

Asali pia inaweza kutumiwa kujipaka. Inapotumiwa kwa njia hii, hutunza ngozi na kuifanya ing'are, huondoa vipele na ugumu wa ngozi ,pamoja na kutibu kule ngozi ilikokatikakatika . Halikadhalika, asali hutibu vidonda. Viwanda vingi vya vipodozi vilevile hutumia asali kama malighafi muhimu katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

(a) Kutokanana na taarifa hii, kwa nini wazee wa zamani waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko watu wa siku hizi? (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(b) Taja matumizi **mawili** ya sukari nyeupe. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(c) Onyesha madhara **matatu** ya sukari nyeupe mwilini. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(d) Taja aina ya sukari iliyo na manufaa mwilini mwa mwanadamu au ueleze ni kwa nini. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(e) Eleza manufaa ya asali: (alama 2)

(i) Ndani ya mwili

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(ii) Nje ya mwili

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

(f) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa: (alama 4)

(i) Hamu na ghamu:……………………………………………………………

……………………………………………………………………………...

(ii) Akina yahe:……………………………………………………………………

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

………………………………………………………………………………………...

(iii) Sugu:…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(iv) Vipodozi:…………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………...

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

2. **<u>UFUPISHO: (ALAMA 15)</u>**

**<u>Soma kifungu kifuatasho kisha ujibu maswali.</u>**

Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha huistawisha ufahamu wetu wa mambo tusemayo.vizuri na katika kuandika hustawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima tujaribu kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusemayo ikiwa imeandikwa hasa huwa ni aina ya lugha ya mazungumzo vilevile. Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza upatikanao katika shule kama vile michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa na haya yote husaida katika matumizi ya lugha.

Ujuzi wa kila siku hutusaida katika maendeleo ya kusoma na ustawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amwemwona ndovu hasa , atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi hata kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile alivyo. Vilevile ujuzi wa kuiona sinema na michoro husaidia sana katika kusoma. Kwa hivyo, kwa njia fulani mambo yote juu ya ujuzi wa kila siku husaidia kufahamu mambo yaliyoandikwa mwanafunzi asemapo. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amesifiwa haya yote ni ujuzi. Wakati ujao mwanafunzi asemapo ju ya mtu ambaye amepatikana na mambo kama hayo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni lakini lugha zote hazina ustawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi lakini katika lugha nyingine karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu. Inabidi mwanafunzi anayejifunza asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma juu ya taaluma fulani anayojifunza. Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya shani, na juu ya mahali pageni ili kupata mambo mengi mbali mbali.

**<u>Maswali</u>**

(a) Fupisha aya za kwanza mbili. (maneno 65 – 70) (alama 9)

**<u>Matayarisho</u>**

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………

...........................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

(b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho. (maneno 30) (alama 6)

**Matayarisho**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Eleza matumizi tofauti ya kiambishi 'ni' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Nitasoma kwa bidii shuleni.

……………………………………………………………………………………………

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(b) Tunga sentensi ukitumia neno 'gani' kama kiwakilishi na kama kivumishi. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(c) Tunga sentensi ukitumia kitenzi 'la' katika hali ya kutendeshea. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(d) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia jedwali. (alama 4)

Walimu shupavu walifunza vizuri lakini wanafunzi hawakupita mtihani.

(e) Onyesha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama2)

Uchaguzi uliofanywa nchini Kenya ulikuwa wa amani.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(f) Bainisha aina za shamirisho katika sentensi: (alama 3)

Shule nzuri ilijengewa wanafunzi kwa matofali.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(g) Eleza sifa **mbili** za sentensi ambatano na utoe mfano mmoja. (alama 3)

……………………………………………………………………………………………

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(h) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo: (alama 2)

(i) Tafakari:…………………………………………………………………………………

(ii) Sujudu:…………………………………………………………………………………

(i) Eleza maana ya shagizo na utunge sentensi moja kuonyesha maana yake. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(j) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya kuamuru katika wingi. (alama 2)

Njoo hapa.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(k) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kipungufu. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(l) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 2)

Asingepigiwa kura, asingekuwa rais wa Kenya.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(m) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi mwafaka. (alama 2)

(i) Mtoto alikula sana.

(ii) Mtoto hakushiba.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(n) Tunga sentensi **moja** ukitumia kihisishi na nomino maalum. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(o) Taja aina **mbili** za mofimu na utolee mfano mmoja mmoja. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(p) Tumia 'amba' rejeshi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mchezaji ninayempenda ni Messi.

…………………………………………………………………………………………………

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

…………………………………………………………………………………………………

(q) Taja sauti **mbili** za nazali. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(r) Andika katika msemo wa taarifa. (alama 2)

"Naapa ya kwamba nitatumikia wananchi wa Kenya na nitakuwa mwaminifu," Rais Mteule alisema.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Nini maana ya Isimu Jamii? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Taja mambo yoyote **matatu** yanayoathiri matumizi ya lugha. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(c) Eleza umuhimu wa sajili. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Taja lahaja **tatu** za Kiswahili na mahali zinakozungumzwa. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com